TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo, Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Ref.No: Taro /P/2022/ A05 **: Swahili Version:** Date: 22nd February 2022

**MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU COSOTA KUTOKUFUATA UTAWALA WA SHERIA KATIKA KUSHUGHULIKIA UVUNJIFU WA HAKIMILI KWA WASANII**

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 24 Novemba 2020, Msanii wa muziki wa kizazi (**Jina limehifadhiwa)** aliwasilisha kwenye **Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (Copyright Society of Tanzania-COSOTA)** malalamiko pamoja na ushahidi juu ya uvunjifu wa hakimiliki wa nyimbo zake. Malalamiko yake yalipokelewa na **COSOTA** kwa ahadi ya malalamiko yale kufanyiwa kazi. Kwa kipindi cha mwaka mmoja, mpaka ilipofika tarehe 13/12/2021 **COSOTA** hawakuweza kushughulikia mgogoro wowote ule kwa mafanikio. Hiyo ilimkatisha tamaa na kumfanya kuamua kuacha kufuatilia haki zake **COSOTA**. Kabla ya **Msanii huyo** kufanya maamuzi ya kuacha kufuatilia haki zake, Taasisi ya Haki za Wasanii **(TARO)** walipata nafasi ya kushuhudia mwenendo mzima wa ushughulikiaji migogoro ya uvunjifu wa Hakilimiliki katika ofisi za **COSOTA**. Ambapo **TARO** iligundua mapungufu makubwa ya kisheria katika ushughulikiaji wa migogoro hiyo .

Imekua kawaida na halali kwa ofisi ya **COSOTA** kushughulikia malalamiko ya uvunjifu wa hakimiliki kwa njia ya maridhiano. Ambapo **COSOTA** wamekua wakiwaandikia barua za wito walalamikaji na walalamikiwa kuja mezani kujadili kwa amani. Endapo Mlalamikiwa akiamua kukataa kuwajibika basi **COSOTA** wanamwambia Mlalamikaji aende mahakamani akafungue kesi bila wao kuchukua hatua yoyote kama sheria inavyowaagiza. Utaratibu huo wamekua wakiutangaza hata kwenye vyombo vya habari kama moja ya hatua zao wanazozichukua pale malalamiko ya uvunjifu wa hakimiliki yanapowafikia.

**HOJA ZA KISHERIA**

**Je kuna uhalali kisheria kwa COSOTA kushughulikia uvunjifu wa Hakimiliki kwa njia ya maridhianao baina ya Mlalamikaji(Msanii) na Mlalamikiwa(Mvunjifu wa hakimiliki)?**

A. Kwa mujibu wa kifungu cha **14** cha sheria iitwayo **Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2019** iliyorekebisha sheria ya Hakimiliki iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.218.R.e. 2002),** Kimeongeza kifungu kingine cha **15A** katika sheria tajwa ya hakimiliki. Kifungu hicho kipya cha **15A** kinaagiza kwamba mtu yoyote mwenye nia ya kutumia haki yoyote inayolindwa na vifungu vya sheria ya hakimiliki anatakiwa kutafuta ruhusa kwa mmiliki wa hakimiliki. Ambapo basi, kwenda kinyume na kifungu hicho cha sheria ni uvunjifu wa hakimiliki.

B. COSOTA imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha **46** cha sheria iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.2018.R.e. 2002)**. Kifungu cha **47** kifungu kidogo **(a)** cha sheria hiyo, kimeipa COSOTA kazi ya kuhamasisha na kulinda maslahi ya wabunifu wa kazi zinazolindwa na Hakimiliki.

C. Kwa mujibu wa **( makosa ya jinai na adhabu zake katika sheria ya hakimiliki)** yaani kifungu cha **42** kifungu kidogo cha **(1)** cha **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.2018.R.e. 2002)**.kama kilivyofanyiwa marekebisho na kifungu cha **15** cha **Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2019,** kinatambua kuwa *mtu yoyote kwa kujua/kufahamu akivunja au akisababisha kuvunjwa kwa haki zinazolindwa na sheria ya hakimiliki ni kosa la jinai na atapaswa kupewa adhabu kama zilivyoorodheshwa na kifungu hicho*. Kwa lugha nyingine, uvunjifu wowote wa hakimiliki ni **kosa la jinai**.

D. Kwa mujibu wa kifungu cha **16** cha sheria iitwayo **Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2019** iliyorekebisha sheria ya Hakimiliki iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.2018.R.e. 2002),** Kimeongeza kifungu kingine cha **42A** katika sheria tajwa ya hakimiliki. Kifungu hicho kipya cha **42A** katika kifungu kidogo **(1)** kinaagiza kuwa *bila kuathiri vifungu vingine vya sheria tajwa ya hakimiliki vinavyohusu adhabu, mtu akikubali kwa maandishi kuwa amefanya kosa la jinai linalopatikana katika sheria ya hakimiliki, Mtendaji Mkuu wa COSOTA au Afisa aliyeruhusiwa na Mtendaji Mkuu wa COSOTA katika kipindi chochote kabla kesi haijaenda mahakamani, anapaswa kufuata taratibu za kumlipisha faini mtu huyo na pia kumlipisha faini na gharama zote COSOTA walizozipata kwa kosa hilo au ada alizotakiwa kulipa kwa mujibu wa sheria.*

E. Kwa mujibu wa Kanuni ziitwazo **Copyright and Neighbouring rights (Compounding Offences) Regulations, 2020. GN.NO.621 OF 2020**, zimeweka utaratibu katika kushughulikia uvunjifu wa hakimiliki, Kanuni zimetumia neno **“shall”** zikimaanisha ni lazima COSOTA wafuate utaratibu ufuatao:-

i. Ikitokea mtu amefanya kosa la jinai linalopaswa kulipishwa faini katika sheria ya Hakimiliki, COSOTA lazima wamtaarifu mtu huyo kwa namna iliyowekwa na sheria kupitia form iitwayo **“Notification Form “N”** iliyooanishwa kwenye jedwali la kanuni hizi. **Rejea** kanuni ya **3** kanuni ndogo **(1)**

ii. Mtu yoyote atakayepokea taarifa iliyoelezwa hapo juu kwenye kanuni ya **3,** anatakiwa ndani ya siku saba tangu apokee taarifa ile, akubali kuwa amefanya kosa lile la jinai au aeleze nia yake ya kujibu mashtaka ya kosa lile la jinai linalomkabili. Kama mtu Yule atakubali kuwa ametenda kosa lile atatakiwa kujaza fomu iitwayo **Admission Form “O”** iliyooanishwa kwenye jedwali la kanuni hizi**.** Kwa kutoa sababu zenye mashiko **COSOTA** wanaweza pokea **Admission Form “O”** hata baada ya kupia siku saba kupita**.** Ikiwa mtu yule ameamua kujibu mashtaka ya kosa lile la jinai linalomkabili, atapaswa kujaza form iitwayo **Intention to Answer Charge Form “P”** iliyooanishwa kwenye jedwali la kanuni hizi. **Rejea** kanuni ya **4** kanuni ndogo **(1),(2)** na **(3)**

iii. Pale ambapo mtu ameamua kujibu mashtaka ya kosa lile la jinai linalomkabili, COSOTA wanatakiwa wawasilishe **Notification Form “N”, Intention to Answer Charge Form “P”** pamoja na taarifa nyingine zinazohusiana kwa **Mkurugenzi wa Mashtaka** kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria (Kufungua kesi ya jinai mahakamani). **Rejea** kanuni ya **5** kanuni ndogo **(1)**

iv. Ikiwa Mtu ameshindwa au amekataa kusaini **Notification Form “N”** itatafsiriwa kuwa amekataa kosa au ameamua kujibu mashtaka ya kosa lile la jinai linalomkabili, Hivyo basi COSOTA watatakiwa kumtaarifu **Mkurugenzi wa Mashtaka** na kuwasilisha taarifa nyingine zinazohusiana kwa **Mkurugenzi wa Mashtaka** kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria (Kufungua kesi ya jinai mahakamani). **Rejea** kanuni ya **5** kanuni ndogo **(2)**

v. Mtu aliyekubali kuwa amefanya kosa la jinai kwa kujaza **Admission Form “O”** atapaswa kulipa faini husika kwa COSOTA, kama COSOTA watakavyoelekeza

F. Kwa mujibu wa kifungu cha **16** cha sheria iitwayo **Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2019** iliyorekebisha sheria ya Hakimiliki iitwayo **Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.2018.R.e. 2002),** Kimeongeza kifungu kingine cha **42A** katika sheria tajwa ya hakimiliki. Kifungu hicho kipya cha **42A** katika kifungu kidogo **(4)** kinaagiza kuwa *kama kosa la jinai litalipishwa faini kupitia kifungu hicho cha* **42A**, *basi faini haitapaswa kuzidi milioni 20.*

## HITIMISHO

**IKUMBUKWE** utaratibu wa sasa, **COSOTA** hushughulikia malalamiko ya uvunjifu wa hakimiliki kwa njia ya maridhiano. Ambapo **COSOTA** wamekua wakiwaandikia barua za wito walalamikaji na walalamikiwa kuja mezani kujadili kwa amani. Endapo Mlalamikiwa akiamua kukataa kuwajibika basi **COSOTA** wanamwambia Mlalamikaji aende mahakamani akafungue kesi bila wao kuchukua hatua yoyote kama sheria inavyowaagiza

Utaratibu huo unaotumiwa na **COSOTA** katika kushughulikia uvunjifu wa Hakimiliki ni kinyume cha taratibu zilizowekwa na sheria. Utaratibu huo haupo kwenye maelekezo ya sheria. Wavunjifu wa Hakimiliki ni waarifu kama walivyowaarifu wengine. Kumuita mezani muarifu na kufanya maridhiano nae katika makosa yake ya jinai ni kinyume na kanuni zilizowekwa na sheria ya Hakimiliki, pia ni kinyume na sheria zinazoongoza mwenendo wa makosa ya jinai. Hivyo basi COSOTA wanapaswa kuheshimu **utawala wa sheria.**

Utaratibu huo wa **COSOTA**, unahamasisha waarifu kuendelea na uarifu kwasababu hawawajibishwi. Pia unawakatisha tamaa wasanii kufuatilia haki zao ambazo ndio ujira wao.

Wasanii walio wengi ni masikini hawana uwezo wa kulipa gharama za wanasheria/Mawakili kupata haki zao mahakamani. Hiyo basi COSOTA kufuata utaratibu uliowekwa na sheria kuna mpunguzia Msanii gharama za kudhibitisha malalamiko yake mbele ya mahakama.

TARO tunalaani vitendo vya COSOTA kutokuwajibika katika **kuheshimu utawala wa sheria** na **kulinda maslahi ya wasanii.** Pia TARO tunawataka COSOTA kuheshimu utawala wa sheria na kuacha mara moja kutumia utaratibu unaopingana na sheria katika kushughulikia uvunjifu wa Hakimiliki.

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**